JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI

715

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Muda: Saa 3:30 **Ijumaa, 16 Mei 2014 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, swali **moja (1)** kutoka kila sehemu B, C na D, na maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu E.
3. Sehemu A ina alama arobaini (40), sehemu B, C na D zina alama kumi (10) kila moja na sehemu E ina alama thelathini (30).
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

LIBRARY

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja sababu nne zinazosababisha wengi waliohiji kutolifikia lengo la Hija.

2. Andika mbinu nne alizotumia Mwenyezi Mungu kuwasiliana na waja wake.

3. Toa tofauti mbili kati ya Talaka tatu na Talaka khul.

4. Toa maelezo mafupi juu ya maneno yafuatayo:
   (a) Ihram
   (b) Talbiya
   (c) Tawaf
   (d) Siku za Tashirq.

5. Bainisha sababu nne zinazomfanya mwanadamu ashindwe kuishi bila dini.

6. Eleza kwa kifupi jinsi mfungaji wa swaumu ya Ramadhan anavyofikia lengo la funga kwa kufanya Sunnah zifuatazo:
   (a) Kula na kuchelewesha kula daku.
   (b) Kuzidisha kusoma Qur'an.
   (c) Kusimamisha swala ya usiku ya tarawehe.
   (d) Kuutafuta usiku wa Lailatul- Qadr.

7. Fafanua dhana zifuatazo:
   (a) Azimio la kazi.
   (b) Kumbukumbu za somo (log book).

8. Taja manufaa manne ya maswali ya insha.

9. Andika sifa nne za malengo mahsususi ya somo.

10. Eleza kwa kifupi utakavyofundisha somo la Kutayamamu kwa kutumia zana halisi.

Scanned by CamScanner

SEHEMU B (Alama 10)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

11. Fafanua hoja nne kuonesha tofauti iliyopo baina ya Qur'an na vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu.

12. Eleza mambo manne yaliyojitokeza katika jamii ya Mtume Nuhu (as) yanayoonesha kuwepo kwa Allah (sw).

SEHEMU C (Alama 10)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

13. Bainisha makundi manane ya watu wanaostahiki kupewa zakat.

14. Fafanua hoja nne kuonesha hekima ya Mwenyezi Mungu kutoa ruhusa ya kuoa wake hadi wanne.

SEHEMU D (Alama 10)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

15. Kwa kutumia mafundisho yatokanayo na kazi ya Mtume (saw) ya miaka kumi na tatu katika mazingira ya Makka, eleza mambo manne kuonesha jinsi ya kuhuisha Uislamu katika jamii yako.

16. Eleza mafunzo manne yanayopatikana kutokana na historia ya Nabii Musa (as).

SEHEMU E (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

17. Kwa kutumia mada ya **Kusimamisha Swala**, andaa azimio la kazi katika kipindi cha wiki mbili.

18. Andika malengo mahsusi manne kutoka katika mada ya **Mafunzo ya Hadithi Zilizochaguliwa** na kisha fafanua vitendo vinne vya ufundishaji na ujifunzaji wa mada hiyo.

19. Kwa kutumia mada ya **Historia ya Mitume**, tunga maswali mawili ya kuchagua jibu sahihi huku ukizingatia usahihi wa kisarufi kati ya shina na kila jibu katika swali (onesha jibu sahihi kati ya majibu manne utakayoandika kwenye swali).

20. Fafanua tofauti kati ya Upimaji endelevu na upimaji awali.

Formative 455 Formative

Scanned by CamScanner